## IHRDC — IRB

Kipeperushi hiki kimetolewa na kitengo cha IRB (Institutional Review Board) ambacho ni sehemu ya Kituo cha Utafiti wa Maendeleo ya afya Ifakara (IHRDC), taasisi ambayo imekuwa ikifanya tafiti za afya nchini Tanzania tangu 1957

IRB ni chombo kinachosimamia maadili ya tafiti zinazofanywa chini ya usimamizi wa Kituo. Chombo hiki kinalo jukumu la kupitia nyaraka za tafiti zinazotarajiwa kufanywa na Wanasayansi wa ndani au wa nje wakishirikiana na Kituo na kutoa kibali cha kufanyika kwa tafiti hizo,

Lengo kuu la IRB ni kulinda usalama na utu wa washiriki wa tafiti za afya katika jamii husika . Hii ni kuhakikisha kwamba tafiti zinazofanywa ndani ya Kituo ni salama na hazidhalilishi wala kudhuru washiriki.

---

**Elewa kama kuna madhara ya utafiti na ni mikakati gani imewekwa kuepusha au kupunguza madhara hayo. Na utasaidiwaje endapo madhara hayo yakitokea**

---

Mshiriki wa tafiti za Afya huchangia maendeleo ya afya ya jamii ya leo na ijayo

Tafiti za Afya ni lazima ziwe salama na zenye kulinda hadhi ya mshiriki na jamii kwa ujumla


IFAKARA HEALTH RESEARCH & DEVPT CENTRE (IHRDC)
MIKOCHENI OFFICE, PLOT 463, KIKO AVE
P O BOX 78373
DAR ES SALAAM
Phone: + 255 22 2774756


# MAADILI YA TAFITI ZA AFYA ZINAZOSHIRIKISHA BINADAMU



IFAKARA HEALTH RESEARCH & DEVELOPMENT CENTRE

AFRICA MALARIA NETWORK